**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA**

**KUONGEZA FURSA NA UBORA WA UPATIKANAJI WA ELIMU YA SEKONDARI KWA NJIA MBADALA**

# MUHTASARI WA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI
## PROGRAMU YA ELIMU YA SEKONDARI KWA NJIA MBADALA

**HATUA I & II**

***2026***

Umetayarishwa na kusanifiwa na:

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

S.L.P 20679, **Dar es Salaam**.

Tovuti: **www: iae.ac.tz**

©Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima 2026

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inayoruhusiwa kutolewa, kutunzwa katika mfumo wa kufunguliwa tena au kubadilishwa katika umbo lolote au kwa namna yoyote, kielektroniki, kimakenika, kurudufisha, kurekodi au vinginevyo bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Watu Wazima, S. L. P 20679, Dar es Salaam.

## 1.0 Utangulizi

Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili kwa Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala unajumuisha Hatua ya Kwanza (Sawa na Kidato cha Kwanza na Kidato cha Pili) na Hatua ya Pili (Sawa na Kidato cha Tatu na Nne) iliyoandikwa katika umbo la moduli. Muhtasari huu una vipengele vilivyounganishwa ambavyo vinapatikana pia katika mtaala wa elimu ya sekondari katika mfumo rasmi. Muhtasari huu umeandaliwa ili kuruhusu wanafunzi kumaliza masomo ya elimu ya sekondari katika muda wa miaka miwili. Umesanifiwa kwa ajili ya wanafunzi walio nje ya mfumo rasmi wa elimu ili kuwawezesha kufanya Mtihani wa Cheti cha Elimu ya Sekondari kwa kutumia stadi na ujuzi walioupata, kutumia umahiri na taaluma katika shughuli zao za kila siku. Mtaala huu umetumia mbinu ya Elimu na Mafunzo yanayozingatia umahiri unaotegemea matokeo yanayoonesha kile ambacho mwanafunzi anatarajiwa kufanya baada ya kumaliza masomo.

## 2.0 Malengo ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

a) Kukuza na kuboresha utu wake ili ajithamini na kukuza kujiamini;
b) Kuheshimu tamaduni, mila na desturi za Mtanzania; tofauti za kitamaduni; heshima; haki za binadamu; mitazamo na vitendo vinavyojumuisha;
c) Kuendeleza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra makini, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mitazamo chanya kwa ajili ya maendeleo yake na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;
d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa, zikiwemo utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;
e) Kuendeleza ujuzi wa maisha na kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
f) Kujenga tabia ya kupenda na kuthamini kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji huduma kwa jamii;
g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka, ikiwa ni pamoja na afya na ustawi wa jamii, usawa wa kijinsia, pamoja na usimamizi na uhifadhi endelevu wa mazingira; na
h) Kuendeleza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari

Malengo ya elimu ya sekondari nchini Tanzania ni:

1. Kuongeza uwezo wa kufikiri na kuimarisha maarifa, stadi na mwelekeo alioupata katika ngazi ya elimu ya msingi;
2. Kuimarisha ukuaji na uthamini wa umoja, utambulisho na maadili ya kitaifa, kuheshimu haki za binadamu, amali za kiutamaduni, mila, desturi na wajibu wa kiraia na utayari wa kufanya kazi za aina mbalimbali;
3. Kutoa fursa ya kupata maarifa, stadi, mielekeo, weledi na uelewa katika nyanja teule za mafunzo;
4. Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifiunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, kivitendo, kitaaluma na kitaalamu;
5. Kuwaandaa wanafunzi kwa kuwajengea ujuzi, umahiri na stadi mbalimbali zitakazowawezesha kujiunga na soko la ajira kwa kujiajiri, na kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na
6. Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu katika ngazi mbalimbali.

## 4.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Tanzania

Malengo ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania ni:

a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, ujuzi na mitazamo iliyojengwa katika ngazi ya Elimu ya Msingi;
b) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, tunu za kitaifa, demokrasia, kuheshimu haki za binadamu na kiraia, wajibu na majukumu yanayohusiana na haki hizo;
c) Kukuza hali ya kujiamini na uwezo wa kujifunza katika nyanja mbalimbali, zikiwemo sayansi na teknolojia pamoja na maarifa ya nadharia na ufundi;
d) Kuboresha mawasiliano kwa kutumia lugha ya alama ya Tanzania, mawasiliano ya mguso, Kiswahili na Kiingereza. Mwanafunzi ahimizwe kukuza umahiri katika angalau lugha nyingine moja ya kigeni, kulingana na hali ya shule huria;
e) Kuimarisha uwajibikaji kwa masuala mtambuka ya kijamii, ikiwa ni pamoja na afya, usalama, usawa wa kijinsia na uhifadhi endelevu wa kiakili wa mazingira;
f) Kukuza umahiri na stadi mbalimbali zitakazomwezesha mwanafunzi kujiajiri, kuajiriwa na kuendesha maisha yake kwa kutumia mazingira yake vizuri; na
g) Kukuza utayari wa kuendelea na elimu ya juu ya sekondari na elimu ya juu.

## 5.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala Nchini Tanzania

Malengo ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala ni;

a) Kutoa elimu ya sekondari kwa watoto, vijana na watu wazima ambao hawakuweza kupata fursa katika mfumo rasmi wa elimu;

b) Kukamilisha juhudi za serikali za kufikia elimu kwa wote;

c) Kutoa fursa ya elimu ya sekondari vijana na watu wazima walioacha shule kwa sababu mbalimbali; na

d) Kutoa elimu kwa makundi ya watu wasiojiweza na waliotengwa wakiwemo wasichana.

## 6.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili

Umahiri mkuu na umahiri mahususi wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili hatua ya kwanza na ya pili ni kama ulivyowasilishwa kwenye Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1:** Umahiri mkuu na umahiri mahususi

| **HATUA YA 1** | |
|---|---|
| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** |
| 1.0 Kulinda historia ya Tanzania, urithi na maadili ya Taifa | 1.1 Kuelezea dhana ya Historia ya Tanzania, chimbuko na maadili ya jamii za Kitanzania<br>1.2 Kumudu maarifa na ujuzi wa maadili na urithi wa jamii za Kitanzania<br>1.3 Kutumia maarifa na ujuzi wa historia na urithi kubaini fursa mbalimbali zilizopo katika jamii, kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa taifa. |
| 2.0 Kumudu historia ya jamii za Kitanzania na maadili kabla ya ukoloni | 2.1 Kuchambua mifumo ya kijamii (elimu, afya, utamaduni) iliyokuza maadili ya Kitanzania kabla ya ukoloni<br>2.2 Kuchambua mifumo iliyokuza na kuendeleza uchumi na siasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>2.3 Kutathmini vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni |

| | |
|---|---|
| 3.0 Kumudu Historia ya Tanzania na Maadili wakati na baada ya ukoloni 1890-1966. | 3.1 Kutumia maarifa na ujuzi wa chimbuko na ukuaji wa mfumo wa ukoloni kuelewa uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na mataifa yaliyoitawala<br>3.2 Kutathmini athari za mfumo wa ukoloni kwenye maadili ya jamii za Kitanzania<br><br>3.3 Kuchambua jitahada za jamii za Kitanzania kupinga ukoloni na Maadili ya kikoloni<br><br>3.4 Kuchambua mifumo ya uchumi, siasa, utamaduni, jamii na maadili iliyojengwa 1961-1966<br><br>3.5 Kumudu historia ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar |
| **HATUA YA 2** | |
| 1.0 Kumudu Historia ya Ujenzi wa Taifa na Maadili yake katika kipindi cha 1961-1985 | 1.1 Kumudu Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar<br>1.2 Kuchambua chimbuko la Azimio la Arusha na matokeo yake kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimaadili<br>1.3 Kueleza nafasi ya Tanzania katika kujenga uhusiano wa kikanda |
| 2.0 Kufanya utafiti wa historia na maadili ya Tanzania | 2.1 Kumudu misingi ya utafiti wa kihistoria<br>2.2 Kutumia misingi ya utafiti wa kihistoria kufanya kazi mradi |
| 3.0 Kutathimini Historia ya Tanzania na Maadili wakati wa Uliberali 1986 hadi sasa | 3.1 Kuchambua chimbuko la Uliberali na utandawazi<br><br>3.2 Kuishi maadili mema ya Kitanzania wakati wa Uliberali na utandawazi |
| 4.0 Kumudu muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 4.1 Kueleza muundo na kazi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar<br><br>4.2 Kubaini muundo na kazi za Serikali za mitaa |

## 7.0 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili unajumuisha vipengele vifuatavyo:

i) **Jina la moduli:** Jina la Moduli limetokana na muunganisho wa mada kuu katika somo husika ambazo zinasawiri umahiri utakaofikiwa na mwanafunzi baada ya kujifunza somo husika.

ii) **Umahiri mkuu:** Huu ni umahiri atakaoupata mwanafunzi baada ya kukamilisha kila moduli.

iii) **Umahiri mahususi:** Huonesha ujuzi mahususi atakaopata mwanafunzi kwa kila mada atakayojifunza. Mkusanyiko wa matokeo mahususi ya kujifunza huunda matokeo makuu ya kujifunza.

iv) **Shughuli za ujifunzaji:** Hizi ni shughuli anazotakiwa kuzifanya mwanafunzi katika tendo la kujifunza. Matokeo mahususi ya kujifunza yanafikiwa baada ya kukamilisha shughuli zote za ujifunzaji zilizopendekezwa.

v) **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji:** Kipengele hiki kinaonesha mbinu za kujifunzia zilizogawanywa katika makundi mawili. Mbinu zitakazotumika darasani wakati mwanafunzi yupo na muwezeshaji na mbinu zitakazotumika nje ya darasa wakati mwanafunzi anajifunza peke yake.

vi) **Vigezo vya upimaji:** Katika kipengele hiki lengo ni kupima uwezo wa mwanafunzi katika kujifunza na uwanja mpana wa uchanganuzi wa mbinu na zana za upimaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili ili kupima umahiri wa mwanafunzi.

vii) **Zana/Vifaa vya kujifunzia:** Katika kipengele hiki, zana mbalimbali za kufundishia na kujifunzia zimependekezwa.

**Viii) Muda wa kujifunza:** Katika kipengele hiki, muda wa kujifunza umependekezwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni saa za kujifunza darasani wakati kundi la pili ni saa za kujifunza binafsi. Saa hisi zimependekezwa kulingana na urefu na ugumu wa mada husika. Hata hivyo, inashauriwa kuwa muda wa saa moja utumike kila siku kwa somo katika usomaj

## 8.0 Idadi ya moduli

Muhtasari huu una hatua mbili ambazo hufanya jumla ya moduli sita kama zinavyoonyeshwa hapa chini:

**Hatua ya I**

Moduli 1: Kuchambua Asili na Maadili ya Jamii Za Kitanzania

Module 2: Kutathmini Mifumo ya Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa katika Kukuza Maadili ya Jamii za Kitanzania Kabla ya Ukoloni

Moduli 3: Kuchambua Mifumo ya Kikoloni na Athari zake katika Maadili na Maendeleo ya Tanzania Kabla na Baada ya Uhuru

**Hatua ya II**

Moduli 1: Kuchambua Historia ya Ujenzi wa Taifa na Maadili yake katika kipindi cha 1961-1985

Moduli 2: Kuelezea Historia ya Tanzania na Maadili wakati wa Uliberali, 1986 hadi Sasa

Moduli 3:Kuchanganua Muundo wa Kazi za Serikali ya Jamhuriya Muungano wa Tanzania

## 9.0 Vitabu vya rejea

Mwishoni mwa kila moduli, idadi ya vitabu vimependekezwa kwa ajili ya usomaji zaidi kuhusu moduli nzima.

## MUHTASARI WA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI HATUA YA I

### UMAHIRI WA SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI HATUA YA I

Baada ya kukamilisha kusoma moduli za Hatua ya Kwanza za Historia ya Tanzania na Maadili, Mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa:

1. Kulinda na kumudu Historia ya Tanzania, Urithi na Maadili ya Taifa.

2. Kumudu Historia ya Tanzania na Maadili kabla ya Ukoloni.

3.Kumudu Historia ya Tanzania, Maadili na Ujenzi wa Taifa wakati na baada ya Ukoloni 1890-1966.

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **KUJIFUNZA BINAFSI** | **ANA KWA ANA** | | | **BINAFSI** | **ANA KWA ANA** |
| **1.0 KUCHAMBUA ASILI NA MAADILI YA JAMII ZA KITANZANIA** | 1.1. Kulinda historia ya Tanzania, urithi, na maadili ya Taifa | 1.1 .1 Kueleza dhana ya somo la Historia ya Tanzania, chimbuko na maadili ya jamii za Kitanzania | a) Kufafanua dhana ya somo la Historia ya Tanzania, chimbuko na maadili ya jamii za Kitanzania | **Kutembelea maktaba:** Mwanafunzi anapaswa kutembelea maktaba, kujisomea vitabu na matini mbalimbali zinazohusu dhana ya Historia ya Tanzania, maadii, na asili ya jamii zake. | **i)Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kufanya majadiliano kuhusu asili ya jamii za kitanzania, urithi na maadili ya kitaifa<br><br>**ii) Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kufanya mdahalo kuhusu chimbuko la jamii za kitanzania na maadili yake. | Dhana ya somo la Historia, chimbuko na, maadili ya jamii za Kitanzania imeelezwa kwa usahihi | Matini zenye kuonesha asili ya jamii za Kitanzania.<br><br>Ramani kuonesha mtawanyiko wa jamii za asili halisi<br><br>Vitu vilivyotumiwa na watu wa jamii za asili | Saa 5 | Saa 1 |
| | | | b) Kueleza asili ya jamii za Kitanzania (Wabantu, Wanilo, Wakushito, Wakichembe) | **Ziara**: Mwanafunzi anapaswa kutembelea vyanzo mbalimbali vyenye taarifa za kihistoria kuhusu | **i)Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kufanya majadiliano kuhusu asili ya jamii za kitanzania, urithi na maadili ya kitaifa | Asili ya jamii za Kitanzania zimeelezwa kwa usahihi | | | |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **KUJIFUNZA BINAFSI** | **ANA KWA ANA** | | | **BINAFSI** | **ANA KWA ANA** |
| | | | | asili ya jamii za kitanzania (makumbusho, maeneo ya kihistoria, masimulizi ya mdomo). | **ii)Maswali na majibu**: Waongoze wanafunzi kubaini jamii mbalimbali za kitanzania. | | | | |
| | | | **c**) Kubaini shughuli mbalimbali za makundi ya asili ya jamii za Kitanzania | **Usomaji wa matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini kuhusu shughuli mbalimbali za makundi ya asili ya jamii za kitanzania . | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadili shughuli mbalimbali za makundi ya asili ya jamii za kitanzania. | Shughuli za makundi ya asili ya jamii za Kitanzania zimebainishwa | | Saa 4 | Saa 1 |
| | | | d) Kueleza maadili ya jamii za asili ya Kitanzania | **Fikiri-andika:** Mwanafunzi anapaswa kusoma, kufikiri, na kueleza | **Maswali na majibu**: Waongoze wanafunzi kujibu maswali kuhusu maadili ya jamii | Maadili ya jamii za asili ya Kitanzania yameele | | | |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | | maadili ya jamii za asili ya kitanzania | mbalimbali za asili | zwa kwa ufasaha | | | |
| | | 1.1.2 Kumudu maarifa na ujuzi wa maadili na urithi wa jamii za Kitanzania | a) Kuchambua maadili na urithi wa jamii za Kitanzania | **Usomaji wa matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini na kuandika muhtasari wa alichojifunza. | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadili na kuandika muhtasari wa walichojifunza. | Maadili na urithi wa jamii za Kitanzania yamechambuliwa kwa ufasaha | Ramani kuonesha maeneo yenye urithi wa Tanzania<br><br>Vitu halisi vilivyotumiwa na watu wa jamii za asili | Saa 5 | Saa 1 |
| | | | b) Kueleza matendo ya msingi yanayokuza na kulinda maadili na urithi wa jamii za Kitanzania | **Kutembelea maktaba:** Mwanafunzi anapaswa kusoma na kubaini matendo ya msingi yanayokuza na kulinda maadili na urithi wa jamii za | **Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kufanya madahalo kujadili matendo ya msingi yanayokuza na kulinda maadili na urithi wa jamii za Kitanzania. | Matendo ya msingi yanayokuza na kulinda maadili na urithi wa jamii za Kitanzania yameelezwa kwa ufasaha | | | |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | | kitanzania | | | | | |
| | | 1.1.3 Kutumia maarifa na ujuzi wa historia na urithi kubaini fursa mbalimbali zilizopo katika jamii, kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa taifa. | a) Kubaini fursa mbalimbali zilizopo kwenye urithi wa jamii za Kitanzania | Kutembelea maeneo: Mwanafunzi anapaswa kutembelea na kubaini fursa anuai zilizopo katika maeneo anamoishi zenye urithi wa jamii za Kitanzania. | **Matembezi ya galari:** Waongoze wanafunzi kuziorodhesha fursa, kubandika kwenye kuta za darasa, na kuuliza maswali mbalimbali. | Fursa mbalimbali zilizopo kwenye urithi wa jamii za Kitanzania zimebainishwa | Matini kuhusu fursa kwenye urithi wa jamii za Kitanzania<br><br>Ramani kuonesha maeneo yenye urithi wa Tanzania<br><br>Vitu halisi vilivyotumiwa na watu wa jamii za asili | Saa 5 | Saa 1 |
| | | | b) Kueleza namna fursa zilizopo kwenye urithi wa jamii za Kitanzania zinavyoweza kutumika kukuza uchumi binafsi na | **Uchambuzi wa matini:** Mwanafunzi anapaswa kusoma matini zenye aina mbalimbali za kisamafunzo na kutoa maoni yao | **i)Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili kisamafunzo na kutoa maoni yao kuhusu fursa za urithi na manufaa yake katika jamii za Kitanzania.<br>**ii)Maswali na majibu:** | Fursa zilizopo kwenye urithi wa jamii za Kitanzania zinavyoweza kutumika kukuza | | Saa 6 | Saa 2 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | jamii | kuhusu fursa za urithi na manufaa yake katika jamii za Kitanzania. | Waongoze wanafunzi katika kusikiliza na kuuliza maswali kwa mtaalamu kuhusu namna ya kutumia fursa za urithi katika kukuza uchumi binafsi na jamii. | uchumi binafsi na jamii zimeelezwa kwa ufasaha | | | |
| | | | c) Kueleza njia mbalimbali za kutunza urithi wa jamii za Kitanzania | **Fikiri-andika:** Mwanafunzi anapaswa kufikiri, kuandika, na kuelezea njia mbalimbali za kutunza urithi wa jamii inayomzunguka. | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili na kuelezea njia mbalimbali za kutunza urithi wa jamii za Kitanzania. | Njia mbalimbali za kutunza urithi wa jamii za Kitanzania zimeelezwa kwa ufasaha | | Saa 4 | Saa 1 |
| | | | d) Kuainisha shughuli mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa | **Matembezi ya galari**: Mwanafunzi anapaswa | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili, kisha waelekeze wabandike matokeo ya utafiti | Shughuli mbalimbali za kujenga ushirikiano na | Matini kuhusu fursa mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa kitaifa, | Saa 4 | Saa 1 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | Taifa | kufanya matembezi maeneo mbalimbali na kuandika shughuli mbalimbali za kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa Taifa. | wao na kurekebisha pale palipokuwa na upungufu. | kukuza uchumi wa Taifa zimeanishwa | Picha kuonesha shughuli mbalimbali | | |
| | | | e) Kufafanua namna shughuli mbalimbali zinavyochangia kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa Taifa | **Fikiri-andika:** Mwanafunzi anapaswa kufikiri na kufafanua shughuli mbalimbali zinavyochangia ushirikiano na uchumi wa Taifa. | **Kujadili na kuwasilisha:** Waongoze wanafunzi kujadili kisha kuwasilisha kwenye darasa kwa majadiliano | Shughuli mbalimbali zinavyochangia kujenga ushirikiano na kukuza uchumi wa Taifa zimefafanuliwa kwa ufasaha | | Saa 4 | Saa 1 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **KUJIFUNZA BINAFSI** | **ANA KWA ANA** | | | **BINAFSI** | **ANA KWA ANA** |
| **2.0 KUELEZA MIFUMO YA KIJAMII, KIUCHUMI NA KISIASA KATIKA KUKUZA MAADILI YA JAMII ZA KITANZANIA KABLA YA UKOLONI** | 2.1 Kumudu historia ya Tanzania na maadili kabla ya ukoloni | 2.1.1 Kuchambua mifumo ya kijamii (elimu,afya,utamaduni) iliyokuza na kuendeleza maadili ya jamii za kitanzania kabla ya ukoloni | a) Kubaini mifumo ya kijamii ya Tanzania kabla ya ukoloni | **Uchambuzi wa matini**: Mwanafunzi anapaswa kutembelea maktaba, intaneti, na kusoma matini kuhusu mifumo ya kijamii ya Kitanzania kabla ya ukoloni. | **i)Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili mifumo ya kijamii ya Kitanzania kabla ya ukoloni **ii)Maswali na majibu:** Waongoze wajifunzaji kujibu maswali kuhusu mifumo ya Kitanzania kabla ya ukoloni. | Mifumo ya kijamii za Tanzania kabla ya ukoloni imebainishwa | Picha kuonesha miundo mbinu ya elimu, afya na utamaduni kabla ya ukoloni Ramani kuonesha mtawanyiko wa miundo mbinu elimu, afya na utamaduni kabla ya ukoloni Vitu halisi vilivyotumika kabla ya ukoloni | Saa 5 | Saa 1 |
| | | | b) Kueleza mifumo ya kijamii ya Kitanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni | **Kusoma matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini ,vitabu na magazeti mbalimbali yanayohusu mifumo ya | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadili namna mifumo ya kijamii ya Kitanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni. | Mifumo ya kijamii ya Kitanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni | | Saa 5 | Saa 1 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **KUJIFUNZA BINAFSI** | **ANA KWA ANA** | | | **BINAFSI** | **ANA KWA ANA** |
| | | | | kijamii ya Kitanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni. | | imeelezwa kwa ufasaha | | | |
| | | 2.1.2 Kuchambua mifumo iliyokuza na kuendeleza uchumi na siasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | a) Kubaini mifumo ya kiuchumi na kisiasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | **Uchambuzi wa matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini kutoka katika vyanzo mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu mifumo ya kiuchumi na kisiasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | **Majadiliano**: Waongeze wanafunzi kujadili na kuwasilisha darasani kwa pamoja | Mifumo ya kiuchumi na kisiasa katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni imebainishwa | Matini kuhusu mifumo ya kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni<br><br>Ramani kuonesha maeneo mbalimbali ya jamii za asili za Kitanzania | Saa 5 | Saa 1 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | | | | | | | |
| | | | b) Kueleza jinsi mifumo ya kisiasa na kiuchumi ilivyokuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni | **Uchambuzi wa matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini mbalimbali kutoka maktaba, intaneti kuhusu jinsi mifumo ya jamii za Tanzania ilivyokuza maadili kabla ya ukoloni. | **Majadiliano na uwasilishaji:** Waongeze wanafunzi kujadili na kuwasilisha darasani kwa pamoja kuhusu shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni. | Mifumo ya kisiasa na kiuchumi ilivyokuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni imeelezwa kwa ufasaha | | Saa 4 | Saa 1 |
| | | | c) Kufafanua uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na za Mashariki ya Kati, Mashariki ya | **Kusoma matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini kuhusu uhusiano | **Uchambuzi wa matini**: Kuongoza wanafunzi kusoma matini kuhusu uhusiano wa jamii moja ya Kitanzania na jamii za | Uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na za Mashariki ya Kati, | | Saa 6 | Saa 2 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | Mbali na Ulaya katika kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni | wa jamii moja ya Kitanzania na jamii za Mashariki ya Kati au Mashariki ya Mbali au Ulaya. | Mashariki ya Kati au Mashariki ya Mbali au Ulaya. | Mashariki ya Mbali na Ulaya katika kuendeleza shughuli za kiuchumi na kisiasa kabla ya ukoloni umefafanuliwa kwa ufasaha | | | |
| | | | d) Kutathmini mchango wa mifumo ya kisiasa na kiuchumi katika kukuza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya | **Kusoma matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini na kuchambua faida na hasara za mifumo ya kisiasa na kiuchumi | **Majadiliano:** Kuwaongoza wanafunzi kujadiliana na kuwasilisha darasani kwa majadiliano ya pamoja. | Mchango wa mifumo ya kisiasa na kiuchumi katika kukuza maadili ya jamii za | | Saa 4 | Saa 1 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | **KUJIFUNZA BINAFSI** | **ANA KWA ANA** | | | **BINAFSI** | **ANA KWA ANA** |
| | | | ukoloni | katika kukuza maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. | | Kitanzania kabla ya ukoloni umetathminiwa | | | |
| | | 2.1.3 Kutathmini vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | a) Kueleza hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | **Kusoma na kuandika:** Mwanafunzi anapaswa kusoma matini na kuandika maelezo kuhusu hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadiliana kuhusu hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. | Hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni imeelezwa kwa ufasaha | Matini kuhusu vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.<br><br>Picha ya bidhaa zilizozalishwa na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni.<br><br>Ramani kuonesha maeneo yaliyokuwa ya uzalishaji wa bidhaa kabla ya ukoloni | Saa 4 | Saa 1 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | b) Kubaini vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | **Usomaji wa matini:** Mwanafunzi anapaswa kusoma matini na kuandika maelezo kuhusu hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma na kujadili kuhusu hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. | Hali ya sayansi na teknolojia katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni imeelezwa kwa ufasaha | Picha kuonesha miundombinu ya elimu, afya na utamaduni kabla ya ukoloni<br><br>Ramani kuonesha mtawanyiko wa miundombinu elimu, afya na utamaduni kabla ya ukoloni<br><br>Vitu halisi vilivyotumika kabla ya ukoloni | Saa 5 | Saa 1 |
| **3.0**<br>**KUCHAMBUA MIFUMO YA KIKOLONI NA ATHARI ZAKE KATIKA MAADILI NA MAENDELEO YA** | 3.1 Kumudu historia ya Tanzania, maadili na ujenzi wa taifa wakati na baada ya ukoloni, 1890-1966 | 3.1.1<br>Kutumia maarifa na ujuzi wa chimbuko na ukuaji wa mfumo wa ukoloni kuelewa uhusiano wa kihistoria kati ya Tanzania na mataifa yaliyoitawala | a) Kuchambua chimbuko la ukoloni | **Usomaji wa matini:** Mwanafunzi anapaswa kusoma matini kutoka kwenye vyanzo mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili chimbuko la ukoloni na kuwasilisha darasani kwa majadiliano ya pamoja | Chimbuko la ukoloni limechambuliwa kwa kina | Matini kuhusu chimbuko la mfumo wa ukoloni<br><br>Picha mbalimbali kuonesha watawala na shughuli za wakoloni | Saa 8 | Saa 2 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| **TANZANIA KABLA NA BAADA YA UHURU** | | | | chimbuko la wakoloni | | | | | |
| | | | b)Kubainisha mataifa yaliyoitawala Tanzania na mifumo yake ya kikoloni katika uchumi, utawala na utamaduni | **Usomaji wa matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini na kubainisha mataifa yaliyotawala Tanzania na mifumo yake ya kikoloni katika kiuchumi, kiutawala na kiutamaduni. | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadili na kuandika kwa ufupi kuhusu mataifa yaliyoitawala Tanzania na mifumo yake ya kiuchumi, kiutawala na kiutamaduni. | Mataifa yaliyoitawala Tanzania na mifumo yake ya kikoloni katika uchumi, utawala na utamaduni yamebainishwa | | Saa 6 | Saa 1 |
| | | | c) Kujadili mchango wa mifumo ya kikoloni | **Fikiri-andika:** Mwanafunzi anapaswa | **Mdahalo** : Kugawa wanafunzi kwenye makundi | Mifumo ya kikoloni katika | | Saa 5 | Saa 1 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala | kufikiri na kuandika kuhusu mchango wa mifumo ya kikoloni katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala. | madogo madogo na wajadili mchango wa mifumo ya kikoloni katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yalioyoitawala. | uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala imejadiliwa kwa kina | | | |
| | | 3.1.2 Kutathimini athari za mfumo wa ukoloni kwenye maadili ya jamii za Kitanzania. | a) Kueleza hali ya maadili ya jamii za Kitanzania kipindi ukoloni unaingia | **Usomaji wa matini**: Mwanafunzi anapaswa kusoma matini kuhusu hali ya maadili ya jamii mojawapo ya Kitanzania kipindi cha ukoloni unaingia. | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili hali ya maadili ya jamii mojawapo ya Kitanzania kipindi ukoloni unaingia kisha wafanye uwasilishaji kwa pamoja | Hali ya maadili ya jamii za Kitanzania kipindi ukoloni unaingia imeelezwa | Matini kuhusu athari za mfumo wa ukoloni kwenye maadili ya jamii za Kitanzania | Saa 7 | Saa 2 |
| | | | b) Kuchambua athari za | **Utafiti mdogo**: Mwanafunz | **Uwasilishaji:** Waongoze wanafunzi | Athari za mfumo | | Saa 5 | Saa 1 |

| JINA LA MODULI | UMAHIRI MKUU | UMAHIRI MAHUSUSI | SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI | MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA | | VIGEZO VYA UPIMAJI | ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI | MUDA/SAA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | KUJIFUNZA BINAFSI | ANA KWA ANA | | | BINAFSI | ANA KWA ANA |
| | | | mfumo wa ukoloni katika maadili ya jamii za Kitanzania | i anapaswa kufanya utafiti mdogo katika vyanzo mbalimbali na kuandika maelezo kuhusu athari za mfumo wa ukoloni katika maadili ya jamii za Kitanzania. | kuwasilisha tafiti zao ndogo kuhusu athari za mfumo wa ukoloni katika maadili ya jamii za Kitanzania. | wa ukoloni katika maadili ya jamii za Kitanzania zimechambuliwa kwa kina | | | |
| | | | c) Kubaini maadili yaliyo dumishwa na jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | **Kisa mafunzo:** Mwanafunzi anapaswa kusikiliza kisamafunzo kuhusu maadili yaliyodumishwa na jamii mojawapo ya | **Maswali na majibu**: Waongoze wanafunzi kuuliza maswali kueleza maadili yaliyodumishwa katika jamii nyingine za Kitanzania wakati wa ukoloni | Maadili yaliyodumishwa na jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni yamebainishwa | | Saa 4 | Saa 1 |

| **JINA LA MODULI** | **UMAHIRI MKUU** | **UMAHIRI MAHUSUSI** | **SHUGHULI ZA UJIFUNZAJI** | **MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ZINAZOPENDEKEZWA** | | **VIGEZO VYA UPIMAJI** | **ZANA ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI** | **MUDA/SAA** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
